

CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM



TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI TANGAZO LA UFADHILI WA MASOMO YA M.A. (KISWAHILI) (MARUDIO)

Taasisi ya Taaluma za Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD) kwa kushirikiana na **Kampuni ya ALAF Limited** ina furaha kutangaza ufadhili wa ada kwa wanafunzi **watatu (3)** waliochaguliwa kusoma **Programu ya M.A. (Kiswahili)** katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa Mwaka wa Masomo 2020/2021.

Mwombaji awe na sifa zifuatazo:

1. Awe raia wa Tanzania,
2. Awe mhitimu wa B.A. (Kiswahili) au programu husiani na kufaulu vizuri katika masomo ya Kiswahili. Kipaumbele kitatolewa kwa wahitimu wa B.A. (Kiswahili),
3. Awe na wakia (GPA) usiopungua 3.8 katika shahada ya awali,
4. Awe amepata udahili wa M.A. (Kiswahili) katika CKD,
5. Awe na umri usiozidi miaka 35 wakati anatumia maombi,
6. Awe mhitaji wa ufadhili wa ada,
7. Awe na uwezo wa kujigharimia mahitaji mengine (chakula, steshenari, malazi, utafiti n.k.).

Nyaraka muhimu za kutuma:

1. Barua ya maombi ambayo pia itabainisha uwezo wa kitaaluma wa mwombaji,
2. Nakala ya cheti cha matokeo ya kitaaluma (transcript) ya shahada ya awali,
3. Nakala ya cheti cha kuzaliwa,
4. Maelezo mafupi (ukurasa mmoja) ya kwa nini anahitaji ufadhili wa ada.

Maombi yatumwe kwa:

Mkurugenzi,
Taasisi ya Taaluma za Kiswahili,
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,
S.L.P. 35110,
Dar es Salaam
Baruapepe: iks@udsm.ac.tz

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 18/11/2020.
